

Rosemary Rwebugisa anafanya kazi za kuainisha maeneo ya vyanzo nya maji, kuyatenga na kuyahifadhi kisheria, kudhibiti uchafuzi wa rasilimali za maji na vyanzo vyake pamoja na kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali ya Maji Na. 11 ya Mwaka 2009, kuwezesha uundwaji wa vyombo nya usimamizi wa rasilimali za maji ikiwa ni pamoja na Kamati za Maji za Mabonde madogo (Catchment Committees) na Jumuiya za Watumia Maji na kufuatilia utendaji wa vyombo hiyo pamoja na kutayarisha na kutunza daftari la Watumia Maji la Taifa.

Bi. Rwebugisa ana Shahada ya Uzamili (MSc. *Geo-information Science and Earth Observation specializing in Water Resources and Environmental Management*) kutoka Chuo Kikuu cha ITC nchini Uhollandi, Shahada ya Jiolojia (Bachelors degree (Honours) in Geology) kutoka Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Kabla ya kuteuliwa kwake, amefanya kazi katika Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoriaawamu ya Pili (LVEMP II) kama Mtaalam wa Rasilimali za Maji na kabla ya hapo amefanya kazi katika Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria kama Mhaidrojiolojia ambapo kabla ya kujiunga na Wizara ya Maji alifanya kazi na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Shinyanga.